# Learning by Ear – Girls' Rights

## Episode 03

## Title: Sexual Harassment- A story of Girls' Rights

**Author: Njoki C. Muhoho**
**Editors: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**
**Proofreading: Michael Lawton**
**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters**

**SCENE 1 SCHOOL PLAYGROUND**

Narrator - Male - 30s
Ciro – Female - 15 years
Fatuma - Female - 14 years
Cheptoo - Female - 15 years
Abdi - Male - 16 years
2 boys - Male - 15-18 years

**SCENE 2 LOCAL VILLAGE PATH**

Ciro – Female - 15 years
Cheptoo - Female - 15 years
Fatuma- 14 years

Man at village path - age unimportant

Narrator - Male - 30s

**SCENE 3 BREAKTIME PLAYGROUND**

Ciro – Female - 15 years
Fatuma - Female - 14 years
Cheptoo - Female - 15 years
Abdi - Male - 15 years
Narrator - Male - 30s
2-3 Boys (just for laughter) 14-16 years

**SCENE 4 GIRLS‘ PARLIAMENT-INCLASSROOM**

Teacher Mona – Female - 35 years
Ciro – Female - 15 years
Cheptoo - Female - 15 years
Abdi - Male - 15 years
Fatuma - Female - 14 years
Narrator - Male - 30s
Mixed boys and girls in class (14-16)

**01. INTRO**

**02. MUSIC: THEME MUSIC**

03. **NARRATOR**

Hujambo, na kwa mara nyingine karibu kwa makala ya tatu kwenye mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga maisha yako kuhusu **'Haki za asichana'**.
Katika kipindi kilichotangulia,Wasichana wawili , Ciro,na Cheptoo wamuokoa rafiki yao Fatuma dhidi ya kupashwa tohara. Pia wanajifunza tamaduni ambazo baado zinafuatwa na wachache katika jamii yao na ambazo zinamuathiri Mtoto wa kike.Wasichana hao wanafahamu fika changamoto zinazowakumba na kwa pamoja wanaamua kukabiliana nazo.Bunge la Wasichana pia labuniwa".
Na hivi leo wanapata fursa ya kujadilia suala la kunyanyaswa kimapenzi.

**SCENE 1: SCHOOL PLAY GROUND**

**04. SFX: BELL RINGS. DOORS OPEN AND SLAM**

**05. <u>SOUNDS: STUDENTS NOISE AS THEY FILE OUT OF CLASSROOMS INTO THE PLAY FIELDS</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 06. | **CIRO** | Fatuma!… Fatuma!.. njoo hapa. Nimekuwa nikiwasubiri sana..wewe na Cheptoo. Mwalimu wako leo amekuchelewesha sana darasani? |
| 07. | **FATUMA** | Ndio Ciro, alitaka niwafikie wenzangu baada ya kukosa kuhudhuria shule kwa wiki kadhaa. ….. |
| 08. | **CIRO** | (LAUGHS) Ni kweli, wakati ulipokuwa katika kizuizi cha nyumbani ukisubiri kuolewa.. |
| 09. | **FATUMA** | Usinicheke...! Wewe ni mnene zaidi kuliko mimi?. Kunamaana wazazi wako wanakupa chakula unone ili wakuozeshe? |
| 10. | **CIRO** | Si waona mwenyewe, niko na mapaja ya kuvutia kuwafanya wavulana wasinitoe machoni. |
| 11. | **FATUMA** | Hiyo ndio kazi yao, kutazama tu.. basi! |

**12. <u>SFX: SOUND: NAUGHTY WHISTLING AND CAT CALLS FROM BOYS (studio)</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 13. | **FATUMA** | Aaahh..ni binamuyo Abdi na rafiki zake. Wanampigia mbijnj ….ama ni Cheptoo..? |
| 14. | **CIRO** | (LOUDLY) Cheptoo! Cheptoo! Njoo tuko hapa. |
| 15. | **ABDI** | (FROM AFAR) Heya… Cheptoo.. umependeza na mtindo wako wa kisasa.. hebu nikusongelee. |
| 16. | | **CHEPTOO** (CHEEKILY)Utakula na macho tu Abdi..ehh utaishia kunawa! |
| 17. | **CIRO** | (AMAZED) Cheptoo, Usiwe na mazoea nao hawa wavulana. Si ..si vizuri..wewe ni Mtoto wa kike... |
| 18. | **ABDI** | (NOW CLOSER). Weee wee….Hebu ni kushike… |
| **19.** | **SFX:** | **LOUD SLAP** |
| 20. | **Abdi:** | Ohh..ni moto na laini kabisa. |
| 21. | **CIRO** | (DISGUSTED) Abdi, hata huoni aibu ikifanya hivyo? Huoni haya kumshika msichana nyuma yake! , Abdi?. |
| 22. | **CHEPTOO** | Sasa nifanye nini, yeye na rafiki zake wananipenda! |

23. **CIRO** Hapana , hapana, Chepto… …uliyataka mwenyewe. Lakini si vizuri wanavyofanya.

24. **FATUMA** Cheptoo, ni kweli anayosema CIRO. (PANIC), Sasa wote wanakuja huku, watazame...! watazame wanavyofaya ndimi zao...wanazibingirisha nje huku wakitutazama…yukkk.. za tisha.

**25. <u>SFX: BELL RINGS</u>**

26. **CIRO** Mungu wangu wee, hebu turudi…turudi darasani upesi. Cheptoo.. njoo, fahanya upesi mwengine asije kukushika nyuma yako tena.

27. **CHEPTOO** (DROOLING) Wacha CIRO,..! usiwe mshamba hivyo! Kwani huoni ni mvuto tulionao kwa wavulana.

28. **FATUMA** Ohh Mungu, makalio yetu!

| | | |
|---|---|---|
| 29. | **NARRATOR** | Cheptoo hana habari…!Kinachoendelea hapa ni unyanyasaji wa kimapenzi.Lakini katika mawazo yake, anaona ni mchezo wa kawaida tu, kwa kuwa wanaofanya hivyo ni wavulana wa rika moja..Je ni sawa ? Na wavulana nao wanafahamu wanavyofanya ni unyanyasaji wa kijinsia? Endela kuwa nasi usikie iwapo watakuja kufahamu wanavyofanya ni makosa. |

**<u>SCENE 2 LOCAL VILLAGE PATH</u>**

**30. <u>SFX: SOUND OF NATURE: FOOTWORK ON DIRT PATH</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 31. | **FATUMA** | CIRO, Cheptoo, kweli nyinyi ni rafiki wa dhati.. kila wakati mnanisindikiza nyumbani. |
| 32. | **CHEPTOO** | Fatuma, tuna wasi wasi kusikia umeozwa kwa kibabu wa miaka 70 |
| 33. | **CIRO** | Wewe ni kama Dada yetu mdogo, na tunakujali. |

**34. <u>SFX: SHUFFLE OF FEET AND BUSHES</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 35. | **CIRO** | Hebu tazama..mtazame yule Mwanamume aliyetupita sasa hivi ... yule pale mbele yetu. |

36. **CHEPTOO** Amefanya nini… Ooh… si nilivyo mdhania.

37. **FATUMA** Lakini anajisaidia tu.

**38. <u>SFX: URINATING SOUND</u>**

39. **ALL GIRLS** Yeeeeek…..

40. **FATUMA** Oooh hapana,.asigeuke kuangalia nyuma

41. **CIRO** oooh.. anageuka

42. **CHEPTOO** (AMAZED) … Oh mungu wangu.. sasa anatuonyesha nini...?

43. **FATUMA** Ooooh hapana …Wacha nifunge macho kabla sijapoteza uwezo wa kuona.

44. **CIRO** Ana … ana .. tuonyesha tupu yake… hata haoni aibu kufanya hivyo?

45. **FATUMA** Kwanini bado unamtazama…Si utazama kando basi. Anataka tuone tu…tuone uchi wake.. CIRO, Cheptoo,fungeni macho.

**46. <u>SFX: SMALL STONES RUBBING ON EACH OTHER</u>.**

47. **CHEPTOO** Nifunge macho? Sasa nikifunga nitaweza kuokota mawe?

48. **FATUMA** Mawe ya nini?

49. **CHEPTOO** Ya kumpura nayo. (HEAVES)

**50. SFX: HEAVING. ROCKS LANDING ON SOFT SURFACE.**

**51. SFX: A MALE GRUNT AND PAINFUL GROWL**

52. **SFX: FEET RUNNING AWAY: GIGGLING**.

53. **NARRATOR** Wanatoroka huku wakicheka, lakini mioyoni mwao wanafahamu fika kwamba kitendo walichoshuhudia si cha haki.Je wasichana hawa wanafahamu kwamba wanauwezo wa kukomesha tabia hii. Endelea kusikiliza..

**SCENE 3 BREAK TIME. PLAYGROUND**

**54. SFX: STUDENTS PLAYGROUND NOISES**

55. **CHEPTOO** Fatuma ana nini?Kwani amechelewa tena kutoka darasani. Na hamu sana kumuona akiungana nasi tena shuleni mwaka ujao.

56. **CIRO** Wajua yeye ameachwa nyuma kimasomo na bila shaka anang'ang'ana kuwafikia wenzake. Au (LAUGHS) anaogopa kuona tupu ya Mwanamume mwengine.

**(ALL LAUGH)**

57. **CHEPTOO** Twende darasani. Kuna kitu nataka kuwaonyesha.

58. **CIRO** Kitu kizuri.? Cha kupendeza?

59. **CHEPTOO** Kwanza ...mpaka ukione sivyo.?

**60. <u>SFX: DOOR OPENS AND CLOSES</u>.**

**61. <u>SFX: MUTED CLASSROOM NOISES</u>**

62. **ABDI** (LOUD WHISPER) Wanakuja huku. Kimya. James jifiche chini ya dawati upesi.

63. **CHEPTOO** Subiri nikutolee,nimekificha chini ya dawati langu.

(SCREAMS!)

64. **CHEPTOO** Abdi unafanya nini chini ya dawati langu?

**65. <u>SOUND: LAUGHTER FROM BOYS! CONTINUES THROUGH THE SCENE</u>**

66. **CIRO** Wanafanya nini?

67. **CHEPTOO** (VERY ANGRY) Toka hapo haraka!! Huna aibu …wewe.. wewe..!!

| | | |
|---|---|---|
| 68. | **CIRO** | Cheptoo…Una akili timamu kweli? Wamefanya nini..? Kwanini anaficha uso wake chini ya dawati lako. |
| 69. | **CHEPTOO** | (VERY HURT), Anachungulia chini ya sketi yangu! |
| 70. | **CIRO** | (VERY ANGRY) Abdi, wewe ni Kakakangu lakini sasa unavuka mipaka. |
| 71. | **CHEPTOO** | (VERY ANGRY) Nadhani sasa tuitishe kikao cha Bunge letu la wasichana ili kulijadili suala hili. |
| 72. | **CIRO** | Tuu…. Nitawaita wasichana wengine pamoja na Mwalimu Mona. Lazima tukomeshe tabia hii! |
| 73. | **NARRATOR** | Kuna haja ya kuitisha kikao cha bunge la Wasichana. Naye Mwalimu Mona ataungana nao ili kuwapa ushauri wanaohitaji, mbali na kuongoza kikao hicho.Endelea kusikiliza unapoungana na Bunge hili la Wasichana. |

## SCENE 4 GIRLS PARLIAMENT

74. **TEACHER MONA** Wanafunzi…., kama mujuavyo, Ciro na wenzake wameunda bunge la wasichana kujadilia hoja inayogusia au kuwaathiri Wasichana.Katika bunge hili, Wasichana kutoka madarasa ya ngazi zote wanaalikwa kujiunga nalo.Leo tumemwita hapa pamoja na wavulana. Na muko huru kujadaliana wazi.

Ciro,… wewe ndie ualiyeitisha kikao hiki, sasa tueleze hoja yako.

75. **CIRO** Mimi, napendekeza kuwa wasichana lazima waheshimiwe na pia tukomeshe unyanyasaji wa kimapenzi.

76. **CHEPTOO** Nnaunga mkono hoja hiyo

77. **TEACHER MONA** Tufungue mjadala.Nani ataanza?

78. **CIRO** Ni wiki hii tu, Abdi alipomshika Chepto sehemu zake za nyuma katika hali ambayo… haiwezi kukubalika. Kisha baadaye tunakutana na Mwanamume mmoja akikojoa mbele yetu na kutuonyesha tupu, hata habari hana. Abdi…naye akakutikana akimchungulia Cheptoo chini ya sketi yake.

**79. SOUND: UPROAR: WHISTLING: AMONG BOYS.**

80. **TEACHER MONA** Order.. Order.. Wavulana kama mna jambo la kusema, tafadhali kuna utaratibu hapa. Abdi, unataka kuwajibu wasichana?

81. **ABDI** Wao wenyewe wanataka hivyo.Cheptoo anapenda sana mambo haya. Anataka!.

82. **CHEPTOO** (ANGRY) Mimi...Nilikwambia ufanye.. ufanye mambo haya….? Unawazimu wewe!.

83. **CIRO** (ANGRY)Unataka kumaanisha pia tulimwambia mwanamume yule atuonyeshe uchi wake?

84. **ABDI** Labda pengine mlikuwa mkicheka-cheka tu na kutamani mmuliyokuwa mkiona.Kwanza Cheptoo alikuwa akifurahia tukimtekerenya. Mara anacheka mara anakasirika. Hatumuelewi..! Lazima muwe na msimamo nyinyi wasichana!!!

**85. SFX: GIRLS SCREAMING**

86. **TEACHER MONA** Order! Order! Nyinyi wavulana lazima mkomeshe tabia hiyo!. Huko ni kuwanyanyasa wasichana!

| | | |
|---|---|---|
| 87. | **ABDI** | Mwalimu Mona, lengo letu si ...nikuwafurahisha. |
| 88. | **CIRO** | (ANGRY) Ongea kwa niaba yako binafsi.Yaani unafurahia kutunyanyasa. |
| 89. | **CHEPTOO** | (ANGRY)… Hata sisi. ..sisi wasichana, pia tunaweza kumfanyizia mambo. |
| 90. | **TEACHER MONA** | Order, Order.. haiwezekani!. Si njia bora ya kushughulikia suala hili.Kwanza ni mfahamu unyanyasaji wa kimapenzi ni nini . |
| 91. | **ABDI** | Tueleze Mwalimu Mona!. Tunataka kujua.. tunakotoka na tunakoelekea, na mahali tunapo kwenda kombo. |
| 92. | **TEACHER MONA** | Nisikilizeni kwa makini. Kila msichana au mvulana ana haki yake ya kijinsia. Na huwezi kudharauliwa kwa jinsi ulivyo. Ni lazima sote tuheshimiana. Sawa? Tunaelewana!. |
| 93. | **ALL** | Sawa Mwalimu Mona!. |
| 94. | **TEACHER MONA** | Lakini nini maana ya unyanyasaji wa kimapanzi? Kwanini wengine wanafurahia na wengine kuhisi wanakosewa? |

| | | |
|---|---|---|
| 95. | **ALL** | Tueleze Mwalimu Mona. |
| 96. | **TEACHER MONA** | Wakati Mtu anapokutamka maneno au kukushika sehemu za mwili, kwa namna ambayo haikupendezi huko ni kukunyanyasa!. Kutumia maneno, kufanya vitendo kwa kudhamiria au kimakosa,kwa namna inayoashiria viendo vya mapenzi kinyume na matakwa yako, huo ni unyanyasaji wa kimapenzi.Na hali hii inaweza tu kufafanuliwa kulingana na jinsi anayetendewa visa hivyo atakavyolichukulia jambo hili. |
| 97. | **ABDI** | Lakini hiyo si haki,.Mfano nikimshika Cheptoo na sikukusudia kumuudhi, kwa tafsiri aseme ni unyanyasaji, nitakuwa mashakani?. |
| 98. | **TEACHER MONA** | Haswa, hiyo ni kweli. Lakini kwanza Cheptoo lazima akufahamishe kwamba hafurashwi na kitendo hicho.Akisema hafurahishwi na wewe uendelee kutenda jambo hilo, basi utakuwa unamnyanyasa. |

| | | |
|---|---|---|
| 99. | **CHEPTOO** | Mumesikia nyinyi wavulana, tukisema wacheni kufanya hivyo lazima muache.…! |
| 100. | **TEACHER MONA** | Subiri …subiri kidogo,huu ni msumeno unaokata pande zote mbili.Pia nyinyi wasichana ni sharti mwaheshimu wavulanana, sio kuwadharau au kuwakandamiza!. Wao pia wanahaki zao,mukiwashika katika hali ambayo haiwapendezi pia wanahaki ya kusema….. nini? |
| 101. | **ALL** | Wacha!!! |
| 102. | **TEACHER MONA** | Tena |
| 103. | **ALL** | Wacha!.. Wacha!..Wacha! |
| 104. | **TEACHER MONA** | Na ukiwa nyumbani pamoja na ndugu,jamaa na marafiki, utasema nini? |
| 105. | **ALL** | (LOUDLY) Wacha! wacha! wacha! |
| 106. | **CHEPTOO** | Na je nikisema Sitaki na mwanamume anaendelea kunishikashika shika. |
| 107. | **CIRO** | Unawezo kumshtaki kwa watu walio mbele yako? |
| 108. | **TEACHER MONA** | Kama nani ???? |

109. **CHEPTOO** Wewe Mwalimu Mona

110. **TEACHER MONA** Sawa

111. **CIRO** Au kwa Janet Afisa wa masuala ya jamii.

112. **CHEPTOO** Kwa wazazi na wakubwa zetu

113. **FATUMA** Pia naweza kutoa habari kanisani au msikitini?

114. **TEACHER MONA** Hiyo ni sawa Fatuma?. Msingi ni kumkataza na kisha kutoa habari kuhusu kitendo hicho.Jambo la mwisho, lazima uweze kutofautishe jambo baya na zuri, Mtu anapokushika, kukutazama au kukuzungumzia!. Tunaweza kufanya hivyo?

115. **ALL** Ndio!!!

116. **CIRO** Sasa tumetoa hoja zetu kuhusu mjadala huu. Wale wanaounga mkono wa kukomeshwa kwa unyanyasaji wa kimapenzi weseme *Yeah*!!!

*117.* **ALL** *Yea!*

118. **CHEPTOO** Na wale wanaopinga waseme *Yea!*!.

**SILENCE**

119. **CIRO** Hoja ya leo imepitishwa. Tunasema HAPANA kwa unyanyasaji wa Kimapenzi..

120. **ALL** Komesha unyanyasaji wa kimapenzi.

**121. THEME MUSIC**

## OUTRO

122. **NARRATOR**

Wavulana kwa wasichana wamejifunza mengi kuhusu unyanyasaji wa kimapenzi, na jinsi ya kuheshimiana.

Ungana nao tena kwa kipindi kijacho cha Learning by Ear Noa Bongo jenga maisha yako usikie ni hoja gani zitakazojadiliwa katika bunge hilo.Endapo una maoni au ungepende kukisikiliza tena kipindi hiki, tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.